

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA
MTIHANI WA KUMALIZA MUHULA WA I – KIDATO CHA III
KISWAHILI

MUDA: Saa 3

MEI 2026

Maelekezo

MsomiBora.com

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11)**.
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A, na B, na **maswali mawili (2)** kutoka sehemu C ambapo swali la **kumi (10)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)**, sehemu B ina alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30)**.
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Jina lako kamili** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.
 - (i) Mzee Chikubati alikuwa akimtetea mtoto wake ambaye ni mhalifu, hatimaye mtoto huyo akauawa na wananchi wenye hasira kali baada ya kukutwa akivunja duka la Bwana Bakari. Ni methali ipi inafanana na maelezo haya?
 - A. Mpiga ngumi ukuta huumia yeye
 - B. Aisifuye mvua imemnyea.
 - C. Maji yakimwagika hayazoleki
 - D. Akumulikaye mchana usiku atakuchoma
 - E. Mchelea mwana kulia hulia yeye
 - (ii) Neno “katapila” limeundwa kwa njia ipi ya uundaji wa maneno?

- A. Kutohoa D. Uhurutishaji
- B. Uambishaji E. Ufupishaji
- C. Urudufishaji

(iii) “Nifungie zege mbili zilizokauka vizuri.” Hii ni rejesta ya mahali gani?

- A. Sokoni D. Mafundi ujenzi
- B. Mgahawani E. Mtaani
- C. Shambani

iv. Ipi ni seti sahihi ya vipera vya semi?

- A. Soga, nyimbo na nahau. C. Methali mizungu na vitendawili
- B. Mafumbo, soga, maghani. D. Mashairi, mafumbo na mizungu.
- E. Misemo mafumbo na vigano

v. Dhima kuu ya misimu katika lugha ni ipi?

- A. Kuficha jambo kwa wasiohusika D. Kutambulisha aina za maneno.
- B. Kuongeza ukali wa maneno E. Kuhimiza shughuli za maendeleo. C.
- Kupatanisha maneno

vi. Ni kauli ipi iliyotumika katika uundaji wa neno “nitamfitinisha”

- A. Kutendeanana D. Kutendea
- B. Kutendesha E. Kutendwa
- C. Kutenda

vii. **Seypalm anaendesha bajaji yake polepole.** Kiarifu cha sentesi hii kimejengwa na mfuatano upi wa viambajengo?

- A. Kitenzi kikuu, shamirisho na chagizo
- B. Kiarifu, kiima na chagizo
- C. Nomino, Prediketa, Shamirisho na Chagizo.
- D. Kiima, chagizo na shamirisho
- E. Kitenzi kishirikishi, shamirisho na chagizo.

viii. Kikundi cha maneno kinachoonesha jambo lililotendwa na mtenda katika sentensi hujulikanaje?

- A. Kikundi Kivumishi
- B. Kikundi Kitenzi
- C. Nomino

D. Chagizo

E. Shamirisho.

ix. Njia ipi hutunza sauti pamoja na vitendo vyake katika kuhifadhi kazi ya fasihi simulizi.

A. Kichwani

C. Mikanda ya Filamu

B. Masimulizi

D. Kinasa Sauti

E. Maandishi

x. Kipi kipengele kinachohusu mpangilio wa matukio katika kazi za fasihi?

A. Muundo

C. Wahusika

E. Mtindo

B. Mandhari

D. Lugha

2. Oanisha lahaja katika Orodha 'A' kwa kuchagua herufi ya jina la lahaja husika katika Orodha 'B', kisha andika herufi husika katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A	Orodha B
i. Lahaja inayozungumzwa Pate.	A. Kimakunduchi.
ii. Lahaja inayozungumzwa kusini mwa msumbiji.	B. Kipate.
iii. Lahaja inayozungumzwa kusini mwa Unguja.	C. Kimtang'ata.
iv. Lahaja inayozungumzwa Mombasa.	D. Kivumba.
v. Lahaja inayozungumzwa Jimbo la Shabu Zaire.	E. Kiungwana.
vi. Lahaja inayozungumzwa Tanga.	F. Kimvita.
	G. Kimwani

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Huku ukitumia mifano kuntu. Fafanua vipashio sita (06) vinavyounda kiima katika sentensi za Kiswahili.

4. a) Mzungumzaji wa lugha ni sawa na bendera fuata upepo. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja nne (04).

b) Kwa kutumia mifano fafanua istilahi zifuatazo;

i. Chagizo.

ii. Prediketa.

iii. Shamirisho.

iv. Kiima

v. Kiarifu.

5.a) Kwa kuzingatia kigezo cha upatanisho wa kisarufi, nomino zimegawanyika katika ngeli

12. Andika ngeli za maneno yafuatayo;

- i. Ndoto
- ii. Ugonjwa
- iii. Siafu
- iv. Mahali
- v. Mkutano

b). Bainisha viambishi vya O-rejeshi katika sentensi zifuatazo kwa kupigia mstari kiambishi hicho.

- i. Udongo ulioletwa umekauka.
- ii. Kijana atakayeshinda atapewa zawadi.
- iii. Karatasi zilizookotwa zimetupwa.
- iv. Gazeti lilioletwa limetumika.

6. Chunguza picha ifuatayo kisha jibu swali linalofuata.

bumbuazi 2 fungu la vitu au wadudu: — la nyuki kikundi cha nyuki waliosongamana na kushikana sana. bumbuazi /bumbu'azi/ nm (-) [i-zi-] hali ya kuwa kimya na kutojua la kufanya au kutosikia lisemwalo  butaa, butwaa, mshangao: Pigwa na —; Shikwa na —. bumbura /bu'mbura/ nm (-) [a-wo-] samaki wa maji chumvi mwenye macho manene anayefanana na chewa au mzia lakini mfupi. bumburuk.a /bumbu'ruka/ kt [rie] (-la, —ka, —sha) 1 shtuka ghafla na kwenda mbio k.v. kundi la ndege au wanyama wanapokurupushwa  kurupuka. 2 amka kwa kitisho. 3 julikana au sikhuka: Siri ime—. bumbwi /bumbwi/ pia bwimbwi /bwimbwi/nm (ma-) [li-yo-] unga wa mchele ulioumuliwa na kutiwa sukari, machicha ya nazi na maji kidogo au tui  kizodo.	56 bungo' mwenye kuleta kisirani au maiba  bumu', babewana, babewatoto.  bundi bundi.a /bu'ndia/ kt [rie] (-ka, —ka, —sha)  taz. kunda, via. bunduki /bu'nduki/ nm (-) [i-zi-] silaha ya kufyatulia risasi kwa nguvu  mrau'. (> Kar/Khi)  bunduki
--	---

Unafikiri picha ya bundi na mchoro wa bunduki vinamsaidiaje mtumiaji wa kamusi? Toa hoja sita (6).

7.Soma utungo ufuatao kisha jibu maswali yanayofuata.

1. Titi la mama ni tamu, hata likiwa la mbwa,
Kiswahili ni adhimu, sifayo iliyofumbwa,
Kwa wasiokifahamu, niimbe iliyokubwa,
Titile mama li tamu, tena haliishi hamu.

2. Lugha yangu ya utoto, hata sasa nimekua,

Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,
Ni sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,
Titile mama li tamu, tena haliishi hamu.

MASWALI

- a. Pendekeza kichwa cha shairi kisichozidi maneno matatu.
- b. Neno “titile” limetumia lugha ya kufupisha maneno. Katika ushairi mbinu hii inaitwaje?
- c. Taja vina vya ndani na nje katika ubeti wa pili.
- d. Mapigo ya kimuziki yanayolifanya shairi hilo liimbike ambayo hupimwa kwa idadi ya silabi huitwa?
- e. Kutokana na shairi ulilosoma, ujumbe gani umeupata?

8. Mzee Ramadhani Mbogo wa kijiji cha Bukabile anatarajia kufanya sherehe ya ubatizo wa binti yake aitwaye Nyanjige Mbogo itakayofanyika tarehe 23/05/2026 katika ukumbi wa ANEX HIRE. Wewe kama mtaalam uliyebobea katika taaluma ya uandishi msaidie kuandaa kadi ya sherehe hiyo.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili** tu kutoka sehemu hii. Swali la **kumi (10) ni la lazima**

9. Fafanua mchango wajerumani katika maendeleo ya Kiswahili enzi ya utawala wao. Toa hoja sita (06) na mifano.
10. Maendeleo ya sayansi na teknolojia ni ndumilakuwili kwa fasihi simulizi. Kwa hoja sita thibitisha ukweli wa kauli hii. Toa hoja tatu kwa kila upande.
11. Jifanye wewe ni mwanafunzi unayeshiriki mashindano ya UMISSETA 2026. Andika insha yenye maneno kati ya 250 hadi 300 kuhusu **umuhimu wa michezo kwa mwanafunzi**.